



CSDR
Settlement & Custody

WITO KWA WANAHISA KUFUATILIA MALIPO YA GAWIO

CSD & Registry Company Limited (CSDR) kampuni tanzu ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) inahusika na ulipaji wa gawio kwa wanahisa wa makampuni yafuatayo ambayo yalitangaza kulipa gawio kwa wanahisa wake:

1. **Vodacom (T) PLC**
2. **TOL Gases Limited (TOL)**
3. **TCCIA Investment PLC (TICL)**
4. **Tanga Cement PLC (TCPLC)**
5. **National Investments PLC (NICOL)**
6. **Mkombozi Commercial Bank PLC (MKCB)**
7. **Dar es Salaam Stock Exchange PLC (DSE)**

Tunapenda kuwataarifu wanahisa wote wa makampuni tajwa hapo juu kuwa, mpaka kufikia tarehe ya tangazo hili kuna idadi kubwa ya wanahisa ambao hawajachukua pesa zao za gawio. Hii inatokana na CSDR kutokuwa na taarifa zao za kibenki au namba za simu ambazo zitawezesha kulipa gawio.

Ili kuweza kulipwa gawio, mwanahisa anapaswa kututumia Taarifa za Kibenki (Namba ya Akaunti na Jina la Benki), Namba ya Simu ya Mkononi pamoja na nakala ya nyaraka zifuatazo:

- Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa (CDS Receipt)
- Kitambulisho (kati ya kitambulisho cha taifa, pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kadi mpya ya mpiga kura)

Mwanahisa anaweza kutuma taarifa zake kwa barua au kwa kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za mwanahisa inayopatikana kwenye tovuti yetu www.csd.co.tz na kutuma kwa Sanduku la Posta, barua pepe au WhatsApp kupitia anuani ifuatayo:

Msajili wa Hisa

CSD & Registry Company Limited
Kambarage House, Gorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni
S.L.P 70081
Dar es Salaam
Simu: 0746 160516 / 0677 070414
Barua Pepe: registrar@csdr.co.tz

Ofisi zipo wazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 2 asubuhi mpaka saa 11 Jioni kwa siku za kazi tu.

MKURUGENZI MKUU
CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED (CSDR)